WHAT 0757478868

2026 MIPANGO YA SOMO LA KISWAHILI - GREDI YA 1 - MUHULA WA 3

WIKI YA 1

Somo la 1

SHULE	ENEO LA SOMO	GREDI	IDADI	MUDA
	Kiswahili	1		

MADA KUU: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

MADA NDOGO: Vyakula vyetu - Matamshi bora

MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA: Kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze:

a) Kutambua sauti legwa katika kadi za maneno.

b) Kutamka sauti legwa ipasavyo.

c) Kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano.

SWALI DADISI: Kwa nini ni muhimu kutamka maneno ipasavyo?

VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA:

- Kitabu cha Mwanafunzi: KLB Early Grade Kiswahili Gredi ya 1 (Uk. 101-115)
- Kadi za maneno zenye sauti /j/, /r/, /p/, /f/, /sh/
- Kifaa cha kidijitali (ikiwezekana)

MPANGILIO WA SOMO: Wanafunzi watafanya kazi kama darasa zima na katika vikundi.

UTANGULIZI Mwalimu ataanza somo kwa kuonyesha kadi za maneno zenye sauti legwa kama vile 'jembe', 'papai', 'chai' na 'yai' na kuwaongoza wanafunzi kuyatamka, akisisitiza sauti za mwanzo.

UENDESHAJI WA SOMO Wanafunzi wataongozwa:

HATUA YA 1: Kushiriki katika kutambua sauti legwa /j/, /r/, /p/, /f/, /sh/ kutoka kwenye kadi za maneno zinazohusiana na vyakula.

HATUA YA 2: Kusikiliza kwa makini mwalimu akitamka sauti legwa na maneno yanayohusiana.

HATUA YA 3: Kutamka sauti na maneno waliyosikiliza pamoja na mwalimu na kisha kibinafsi.

HATUA YA 4: Kutumia kifaa cha kidijitali (ikiwepo) kusikiliza matamshi bora ya sauti legwa na kujaribu kuiga.

HITIMISHO Mwalimu atahitimisha somo kwa mchezo wa kutambua sauti. Atatamka neno na wanafunzi watataja sauti legwa iliyomo.

SHUGHULI ZA ZIADA Wanafunzi watafute na wataje majina ya vyakula vitatu wanavyovijua nyumbani.

TAFAKARI KUHUSU
SOMO .....
.....
.....

Somo la 2

SHULE	ENEO LA SOMO	GREDI	IDADI	MUDA
	Kiswahili	1		

MADA KUU: KUSOMA

MADA NDOGO: Vyakula vyetu - Kusoma kwa ufasaha

MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA: Kufikia mwisho wa somo, mwanafunzi aweze:

a) Kutambua sauti legwa katika kifungu chepesi cha hadithi.